JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MJI GEITA

**Kumb. Na. CA.225/252/01/19** **TAREHE: 28/06/2023**

# YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MKATABA KATIKA HOSPITALI YA HALMASHUARI YA MJI GEITA.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Geita anawatangazia wananchi kuwa kuna nafasi ya kazi za mkataba katika Hospitali ya Halmashauri ya Mjii Geita kwa mpango wa "National Health Workforce Volunteering Guideline".

## 1.0 MUUGUZI DARAJA II - NAFASI TISA (09)

### 1.1 MAJUKUMU YA KAZI.

i. Kufanya kazi za kiuguzi za kuhudumia wateja katika jamii, hospitali na sehemu zote zinapotolewa huduma za afya.
ii. Kusimamia na kuratibu kazi zote za wahudumu wa afya katika sehemu yake ya kazi
iii. Kukusanya takwimu na kutayarisha taarifa za utendaji wake wa kazi
iv. Kutoa huduma kwa wagonjwa majumbani.
v. Kutoa ushauri nasaha
vi. Kutoa huduma za kinga na uzazi wa mpango
vii. Kutoa huduma za uzazi na afya ya mtoto
viii. Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
ix. Kufuatilia utunzaji wa vitendea kazi katika maeneo yake ya kazi
x. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

**SIFA ZA MUOMBAJI:**

i. Awe na cheti cha Uuguzi cha miaka miwili kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali na kuandikishwa (Enrolled) na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.
ii. Awe na umri wa miaka 18 hadi miaka 45.
iii. Awe anajitolea/alishawahi kujitolea Vituo vya kutolea huduma za Afya katika Halmashauri ya Mji Geita.
iv. Mwombaji awe na Elimu kidato cha Nne (IV) au cha sita (VI).
v. Awe ni raia wa Tanzania.
vi. Mwombaji awasilishe na wasifu wake (CV) na picha moja (passport size)
vii. Mwombaji awasilishe nakala ya cheti cha kuzaliwa pamoja na kitambulisho cha Taifa.
viii. Awasilishe nakala ya vyeti vya taaluma pamoja na leseni.
ix. Ambatanishe na barua ya kujitolea.

## 2.0 AFISA MTEKNOLOJIA DAWA MSAIDIZI DARAJA II – NAFASI MOJA (01)

### 2.1 MAJUKUMU YA KAZI.

i. Kuainisha, kuandaa na kuagiza mahitaji ya dawa na vifaa tiba katika eneo lake la kazi.
ii. Kugawa dawa na vifaa tiba kwa wagonjwa na watumishi Kuchanganya dawa
iii. Kuhifadhi dawa na vifaa tiba
iv. Kuelimisha jamii kuhusu matumizi sahihi ya dawa Kukagua dawa, vifaa tiba kemikali,
vitendanishi na vipodozi katika eneo lake la kazi
v. Kutoa taarifa juu ya madhara yatokanayo na matumizi ya dawa.
vi. Kuratibu kazi za kamati ya dawa ya hospitali
vii. Kuandaa taarifa ya matumizi ya dawa na vifaa tiba
viii. Kufanya uchunguzi wa ubora wa dawa, vifaa tiba kemikali, vitendanishi na vipodozi
ix. Kufanya kaguzi mbalimbali katika sehemu zinazohifadhi dawa.
x. Kusimamia utendaji wa kazi watumishi walio chnini yake
xi. Kutunza kumbukumbu za dawa na vifaa tiba
xii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

### SIFA ZA MWOMBAJI.

i. Awe mwenye AStashahada katika fani ya Uteknolojia katika fani tajwa hapo juu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Mabaraza pale inapohusika.
ii. Awe na umri wa miaka 18 hadi miaka 45
iii. Awe anajitolea/alishawahi kujitolea Vituo vya kutolea huduma za Afya katika Halmashauri ya Mji Geita.
iv. Mwombaji awe na Elimu kidato cha Nne (IV) au cha sita (VI).
v. Awe ni raia wa Tanzania.
vi. Mwombaji awasilishe na wasifu wake (CV) na picha moja (passport size)
vii. Mwombaji awasilishe nakala ya cheti cha kuzaliwa pamoja na kitambulisho cha Taifa.
viii. Awasilishe nakala ya vyeti vya taaluma
ix. Ambatanishe barua ya kujitolea.

## 3.0 AFISA MTEKNOLOJIA MAABARA MSAIDIZI DARAJA II – NAFASI (04)

### 3.1 MAJUKUMU YA KAZI.

i. Kupima sampuli zinazoletwa maabara.
ii. Kuhifadhi sampuli zinazotakiwa kufanyiwa uchunguzi au kupelekwa Maabara za ngazi za juu.
iii. Kufanya kazi za ukaguzi wa maabara, vitendanishi, vifaa, kemikali na hifadhi ya kemikali
iv. Kuweka kumbukumbu za maabara ambazo zimepatikana wakati wa uchunguzi.
v. Kufundisha watumishi walio chini yake.
vi. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

**SIFA ZA MUOMBAJI:**

i. Awe na AStashahada katika fani ya Uteknolojia katika fani tajwa hapo juu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Mabaraza pale inapohusika.
ii. Awe na umri wa miaka 18 hadi miaka 45
iii. Awe anajitolea/alishawahi kujitolea Vituo vya kutolea huduma za Afya katika Halmashauri ya Mji Geita.
iv. Mwombaji awe na Elimu kidato cha Nne (IV) au cha sita (VI).
v. Awe ni raia wa Tanzania.
vi. Mwombaji awasilishe na wasifu wake (CV) na picha moja (passport size)
vii. Mwombaji awasilishe nakala ya cheti cha kuzaliwa pamoja na kitambulisho cha Taifa.
viii. Awasilishe nakala ya vyeti vya taaluma pamoja na leseni.
ix. Ambatanishe barua ya kujitolea.

## 4.0 MHUDUMU CHUMBA CHA MAITI – NAFASI MBILI (02)

### 4.1 MAJUKUMU YA KAZI.

i. Kufanya usafi wa chumba cha kuhifadhia maiti
ii. Kupokea, kuosha na kutunza maiti
iii. Kazi nyingine atakazopangiwa na kiongozi wake wa kazi.

**SIFA ZA MWOMBAJI:**

i. Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne waliopata mafunzo ya mwaka mmoja katika fani ya afya.
ii. Awe na umri wa miaka 18 hadi miaka 45
iii. Awe ni raia wa Tanzania.
iv. Awasilishe nakala vyeti vya taaluma

## 5.0 AFISA TEHAMA MSAIDIZI – NAFASI MOJA (01)

### 5.1 MAJUKUMU YA KAZI.

i. Kusimamia mifumo ya Tehama katika Hospitali.
ii. Kufanya matengenezo ya vifaa (Computer, CCTV Camera, Photocopy Machine na Printer)
iii. Kusimamia mifumo ya Got-Homis katika Hospitali.

**SIFA ZA MUOMBAJI:**

i. Awe na Stashahada katika fani ya Computer Science / Information tenchnology katika fani tajwa hapo juu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.
ii. Awe na umri wa miaka 18 hadi miaka 45
iii. Mwombaji awe na Elimu kidato cha Nne (IV) au cha sita (VI).
iv. Awe ni raia wa Tanzania.
v. Mwombaji awasilishe na wasifu wake (CV) na picha moja (passport size)
vi. Mwombaji awasilishe nakala ya cheti cha kuzaliwa pamoja na kitambulisho cha Taifa.
vii. Awasilishe nakala ya vyeti vya taaluma.
viii. Ambatanishe barua ya kujitolea.

**UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI**

Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **12/07/2023** saa **9:30** Alasiri. Maombi yatumwe kwa njia ya Posta kwa **S.L.P 384, Geita** au yaletwe Masjala ya Halmashauri ya Mji Geita, watakaokidhi vigezo watajulishwa kwa simu na katika mbao za matangazo ili kuweza kuja kwenye usaili.

Tangazo hili limetolewa na,

*Lee Joshua Kyangalla*
**KAIMU MKURUGENZI WA MJI.**



MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
GEITA.